

**HOTUBA YA WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA
MICHEZO, MHE. DKT HARRISON MWAKYEMBE (MB), KATIKA
HAFLA YA KUFUNGUA KITUO CHA URITHI WA UBUNIFU MAJENGO
NA UTALII KATIKA JIJI LA DAR ES SALAAM,
TAREHE 30 JUNI, 2017**

Balozi wa Umoja wa Nchi za Ulaya, Mhe. Roeland Van De Geer,
Mstahiki Meya wa Jiji la Dar es Salaam, Mhe. Isaya Mwita Charles,
Waheshimiwa Madiwani wa Dar es Salaam,
Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam, Bibi Sipora Liana
Rais wa Jumuiya ya Wasanifu Majengo Tanzania, Architect Henry Mwoleka
Mkurugenzi Mkuu wa Kituo cha Urithi wa Ubunifu Majengo, Bibi Aida
Mulokozi,
Wageni waalikwa,
Waandishi wa Habari,
Mabibi na Mabwana,

Awali ya yote ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa kupewa heshima hii ya kufungua Kituo cha Urithi wa Ubunifu Majengo katika Jiji la Dar es Salaam ambacho kipo katika jengo hili la kale la Old Boma lenye historia kubwa katika nchi yetu ambalo limefanyiwa ukarabati kwa kiwango cha juu na kuwa mfano wa uhifadhi endelevu na kituo cha kutangaza historia ya ukuaji wa miji yetu kanda ya Afrika mashariki.

Ningependa pia kuchukua fursa hii kuipongeza Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kwa kulitoa jengo hili liweze kutumika kama Kituo cha Urithi wa Ubunifu wa Majengo na Utalii. Aidha, nimefurahishwa na juhudhi zinazofanywa na Halmashauri hiyo za kuvitangaza vivutio vya utalii vya Jiji hilo, kuogeza pato la Jiji kupitia shughuli za utalii na mipango yake ya kuwa na mabasi ya Halmashauri ya kuhudumia watalii.

Waheshimiwa madiwani, wageni waalikwa, mabibi na mabwana,

Jumuiya ya Wabunifu Majengo Tanzania na washirika wake wanastahili pongezi kubwa kwa kuanzisha mpango huu wa kuelimisha, kutunza na kudumisha majengo ya kale ambayo utakua ukisaidia kukuza na kuendeleza utalii katika Jiji la Dar es Salaam na Tanzania kwa ujumla.

Kwa kazi kubwa iliyofanywa na Jumuiya ya Wabunifu Majengo Tanzania kwa kuanzisha na kusimamia mpango huu, ninaamini kwamba nchi zetu za Afrika Mashariki zitapata nafasi kubwa ya kubadilishana mawazo na uzoefu utakaoisaidia miji yetu kutatua changamoto mbalimbali zinazosababisha majengo ya kale kuachwa bila kutunzwa, kubomoka, kubomolewa na kuanguka bila ya kuwa na usimamizi wa dhati katika utunzaji wa majengo hayo.

Waheshimiwa madiwani, wageni waalikwa, mabibi na mabwana,

Dar es Salaam ni mji ambao unakua kwa haraka na shughuli za ujenzi wa majengo na miundombinu ni kubwa. Nisingependa kuona shughuli hizo zikiathiri majengo ya kale bila sababu za msingi zilizoridhiwa na Serikali. Nitumie fursa hii kuwashukuru wabunifu majengo, washirika wake wote na wataalamu wote wanaohusika katika shughuli za ujenzi zinazookoa majengo ya kale, kwetu ni faraja kuu.

Aidha, nitoe wito kwa wananchi na wadau wote kuwa na mawazo ya utunzaji wa majengo ya kale badala ya uvunjwaji wa majengo hayo kama inavyoendelea katika Jiji la Dar es Salaam bila kupata vibali vya mamlaka husika Serikalini. Kama watu wote na wadau wote wangelikuwa na mawazo chanya na endelevu ya utunzaji wa majengo na minara ya kale iliyopo hapa nchini kama wenzetu wa Jumuiya ya Wabunifu wa Majengo na washirika wake majengo ya kale yasingevunjwa na kupotea kwa haraka.

Waheshimiwa madiwani, wageni waalikwa, mabibi na mabwana,

Ni dhahiri kwamba wananchi sasa wataweza kufahamu umuhimu wa kutunza na kuhifadhi majengo ya kale kutokana na elimu watakayoipata kutoka kwenye kituo hiki. Kwa hiyo, ninawaelekeza kuendeleza juhudini za kikitangaza kituo hiki ili wananchi na wadau wa ndani na nje ya nchi waweze kikitumia na kufaidika na elimu itakayotolewa katika kituo hiki kilichopo katika jengo hili la kale la Old Boma.

Aidha, nitoe wito kwa Jumuiya ya Wasanifu Majengo Tanzania kushirikiana na taasisi za ndani na nje ya nchi kutunza majengo na sehemu za kale hapa nchini na Afrika Mashariki katika utekelezaji wa mipango yenu ya kuanzia Jiji la Biashara la Dar es Salaam kupitia Kituo hicho ili muweze kuimarisha juhudini za kudumisha na kukuza utamaduni kwa kuyaboresha majengo ya kale.

Kwa upande wa Mamlaka za Serikali za Mitaa katika Jiji la Dar es Salaam ninawasisitiza kusimamia sheria na kushughulikia kero zinazotokana na udhaifu wa kutosimamia sheria ambazo kimsingi zingeweza kusaidia kuimarisha usalama na kutunza mazingira ya majengo yote ya kale na majengo ya kisasa ambayo kama nilivyooleza majengo hayo ni sehemu kubwa ya vivutio vya utalii nchini.

Waheshimiwa madiwani, wageni waalikwa, mabibi na mabwana,

Baada ya kusema hayo, ninarudia kuwashukuru kwa kunikaribisha katika ufunguzi wa Kituo hiki na sasa ninatamka kwamba **Kituo hiki endelevu cha urithi wa ubunifu wa majengo na utalii katika Jiji la Dar es Salaam kimefunguliwa rasmi.**

Asanteni sana